# Ramadhani

## Mwezi wa Ramadhani **unaingiaje?**

## Kuingia kwa mwezi wa Ramadhani kunathibiti **kwa mojawapo ya mambo mawili**

### 1 Kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Fungeni kwa kuonekana kwake na fungueni kwa kuonekana kwake".* (Bukhariy 1800, Muslim 1081). Maana ni kuonekana kwa mwezi muandamo. Iwapo **Muislamu mwenye akili timamu, balehe,** muadilifu, anayekubalika kwa uzoefu wake na uaminfi wake atauona mwezi muandamo wa Ramadhani, itakuwa imethibiti kuingia kwa mwezi na itakuwa lazima kwa watu kuanza kufunga.

### 2 Kukamilika kwa siku thalathini za mwezi wa Shabani.

**Kwa sababu mwezi muandamo ni ama siku ishirini na tisa au thalathini, na hauwi zaidi ya hapo.** Zikikamilika siku thalathini za mwezi wa Shabani, maana yake ni kwamba mwezi wa Ramadhani umeanza. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Fungeni kwa kuonekana kwake na fungueni kwa kuonekana kwake. Ikiwa umefunikwa kwenu kwa mawingu, basi kamilisheni hisabu ya siku thalithini za Shabani"*. (Bukhariy 1810, Muslim 1081).

**Iwapo Waislamu ni wachache** katika nchi isiyokuwa ya **Kiislamu, watafuata vile vyombo na taasisi za Kiislamu zinavyosema.** Vyombo na taasisi hizi za Kiislamu ikiwa zitatafautiana, ni juu ya Muisamu kuifuata taasisi ya Kiislamu iliopo katika mji wake ambao anaishi au Msikiti wa Ijumaa ambao upo mjini kwake au msikiti ambao anasali. Ajitahidi kufuata Jamaa (kundi) kadiri awezavyo.

## **Rejea ni nini katika** kuingia kwa Ramadhani na Idi?

Ni tangazo rasmi la nchi ambayo Waislamu wanaishi.
Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, anasema kuwa: *"Kufungua kweni ni siku mnapofungua na kuchinja kwenu (mnyama wa Udh-hiya) ni siku mnapochinja"*. (Abudaud 2324, Tirmidhiy 697).

## Ubora wake

### **Usiku** wenye hadhi kubwa.

ambao Mwenyezi Mungu katika kitabu chake ameuelezea kuwa jambo jema linalofanywa katika usiku huo ni bora zaidi kuliko kulifanya katika nyakati nyingine nyingi. Amesema kuwa: ***"Usiku wa hadhi ni bora zaidi kuliko miezi elfu".*** (Sura Alqadri, aya 3). Mwenye kusimama (kwa kusali) katika usiku huo kwa sababu ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kutaraji malipo kutoka kwake, atasemehewa dhambi zake zilizopita. Na huo ni **usiku katika usiku wa siku kumi za mwisho** za mwezi wa Ramadhani. Unaanza wakati wa Adhana ya Magharibi na unakwisha kwa kuchomoza kwa Alfajiri. Hakuna ajuae hasa wakati wake. Limefanyika hilo ili tufanye juhudi katika usiku wa siku zote.

#### Na maana ya miezi elfu

imesemekana kuwa maana yake ni hivyo hivyo ambapo ni miezi 1000.

Na imesemekana pia kuwa maana yake ni kuonesha kiwango cha juu cha ukubwa wa malipo yake na ubora wake. Elfu hutumika katika kuonesha ongezeko la kiwango cha juu. Na fadhila za Mwenyezi Mungu hazina kikomo.

### **Kushuka kwa** Qur'ani.

Ni mwezi ambao Mwenyezi Mungu ameupa sifa ya kipekee ya kushuka kwa Qur'ani, kitabu kikubwa na kitukufu sana. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Mwezi wa Ramadhani ambao imeshuko humo Qur'ani ikiwa ni muongozo kwa watu na ni ufafanuzi wa muongozo na upambanuzi. Kwa hiyo, yeyote miongoni mwenu atakayekuwemo katika mwezi huo aufunge"*. (Sura Albaqara, aya 185)

### **Milango ya peponi inafunguliwa** na mashetani wanafungwa.

Katika mwezi huu milango ya peponi inafunguliwa na mashetani wanafungwa. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Inapoingia Ramadhani, milango ya peponi inafunguliwa na milango ya motoni inafungwa na mashetani wanafungwa pingu".* (Bukhariy 3103, Muslim 1079). Mwenyezi Mungu amewawekea waja wake mazingira mazuri ya kurejea kwake kwa kutenda mema na kuacha maasi.

### Kusamehewa dhambi kwa sababu ya kufunga na kusali

Mwenye kufunga saumu katika mchana wa Ramadhani na kusimama usiku wake kwa kusali atasamehewa dhambi zake zilizoita.

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwenye kufunga Ramadhani kwa (sababu ya) kuamini na kutaraji malipo kwa Allah atasamehewa dhambi zake zilizopita"*. (Bukhariy 1910, Muslim 760).

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwenye kusimama Ramadhani (kwa kusali) kwa (sababu ya) kuamini na kutaraji malipo kwa Allah atasamehewa dhambi zake zilizopita"*. (Bukhariy 1905, Muslim 759).

## Kwa nini umeitwa Ramadhani?

Katika kipindi cha kabla ya Uislamu, Waarabu walipotaka kuyatoa majina ya miezi kutoka katika lugha za zamani wali ipa miezi majina ya nyakati za miezi hiyo. Mwezi huu ukaafiki kuwa katika kipindi cha joto kali na, kwa hiyo, ukaitwa **Ramadhani kutokana na neno "Ramdhaa" lenye maana ya joto kali.**
Kama ambavyo pia mwezi wa Rabii Awwal (Mfungosita) na Rabii Thaniy (Mfungosaba) ulivyoitwa hivyo kwa sababu ya kuafikiana na kipindi cha Rabii (msimu wa mimea na mazao kustawi = masika).

## Historia yetu katika **Ramadhani**

Ramadhani, kupitia historia, imesheheni matukio mengi ya ushindi na ya kihistoria. Miongoni mwa matukio hayo ni haya yafuatayo:

### Vita vya Goliathi — H 685

Ni vita vikali vilivyoumaliza uvamizi wa Wamongolia kwa nchi za Waislamu chini ya uongozi wa Mfalme Qutuz na Kamanda Berbs. Goliathi ipo kaskazini ya nchi ya Palestina. Vita hivi vilitokea tarehe 25 Ramadhani, mwaka 685 Hijiria sawa na mwaka 1260 Miladia.

### Ukombozi wa Amuriyah — H 223

Pale kiongozi wa utawala wa Abasia, Almuutasim alipoliongoza jeshi kubwa kwa ajili ya kumtetea mwanamke wa Kiislamu aliyeomba msaada kwake kutokana na mashambulizi ya majeshi ya Wapiganaji Wakristo wa Vita vya Msalaba chini ya uongozi wa Theofile Mikael. Almuutasim aliuzingira mji wa Amuriyah ambao ni mji uliopo Uturuki hivi sasa na, Mwenyezi Mungu kupitia kwake, akaukomboa mji huo (tarehe 17 Ramadhani, 223 Hijiria, sawa na 15 Agosti, 838 Miladia).

### Ukombozi wa kisiwa cha Sicily — H 201

Kisiwa hiki kipo kusini mwa Italia. Kilikombolewa na kiongozi na mwanachuoni Asad Bin Alfuraat, Mwenyezi Mungu amrehemu, na ambaye alikufa shahidi kufuatia jeraha alilolipata katika vita. Utawala wa Kiislamu ulidumu hapo kwa zaidi ya karne mbili na nusu. Waislamu walisambaza elimu, ustaarabu na tasnia mbali mbali za ujenzi. Ukombozi wa kisiwa hicho ulikuwa tarehe 9 Ramadhani, mwaka 212 Hijiria, sawa na 6 Desemba, mwaka 827 Miladia.

### Ukombozi wa nchi ya Andalusia (Hispania) — H 92

Chini ya uongozi wa Tariq Bin Ziad Waislamu walipata ushindi baada ya mapambano makubwa na Mfalme Dhirik, ambapo ilikuwa mwanzo wa enzi za elimu, ustaarabu na kuvumiliana kwa muda wa karne nane. Hiyo ilikuwa tarehe 28 Ramadhani, mwak 92 Hijiria, sawa na tarehe 19/07/711 Miladia.

### Ukombozi wa Makka — H 8

Pale Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipoingia mjini humo kwa amani bila ya vita huku akiwa ameinamisha kichwa chini kwa ajili ya utiifu na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, na akisoma: *"Sema: imekuja haki na batili imeondoka. Kwa yakini, batili ni yenye kuondoka"*. (Sura Albaqara, aya 183). Hiyo ilikuwa tarehe ishirini ya mwezi wa Ramadhani, mwaka wa nane wa Hijiria, sawa na 10/1/630 Miladia.

### Mwanzo wa Ramadhani imefaradhishwa funga — H 2

Mwanzo wa Ramadhani ilifaradhishwa funga katika mwaka wa pili wa Hijiria, sawa na mwaka 624 Miladia. Hilo ni kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: *"Enyi ambao mmeamini, imefaradhishwa kwenu funga kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwepo kabla yenu ili mpate kuwa wachamungu"*. (Sura Albaqara, aya 183).

### Vita vya Badri — H 2

Waislamu katika vita vya Badri walipata ushindi dhidi ya makafiri wa Kikuraish, na Qur'ani kuiita siku hiyo "Siku ya Upambanuzi" kwa sababu ni vita vya kwanza katika Uislamu baina ya haki na batili. Vilitokea katika siku ya saba ya mwezi wa Ramadhani katika mwaka wa pili wa Hijiria, sawa na 13/3/624 Miladia.

### Kushuka kwa Qur'ani — ق.هـ ١٣

Kushuka kwa Qur'ani kwa Mtume wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kulianza katika pango la Hiraa la mlima unaojulikana hivi sasa kama Mlima Nuur uliopo karibu na mji wa Makka pale Jibrili, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, alipoteremsha sura ya mwanzo isomekayo: *"Soma kwa jina la Mola wako ambaye ameumba"*. (Sura Al-alaq, aya 1). Hilo lilitokea katika siku ya Jumatatu tarehe 21 Ramadhani sawa na Agosti 10, mwaka 610 Miladia, katika mwaka (13) kabla ya Mtume kuhamia Madina.

| | |
|---|---|
| 1260 Miladia | Vita vya Goliathi |
| 838 Miladia | Ukombozi wa Amuriyah |
| 817 Miladia | Ukombozi wa kisiwa cha Sicily |
| 711 Miladia | Ukombozi wa nchi ya Andalusia (Hispania) |
| 630 Miladia | Ukombozi wa Makka |
| | Vita vya Badri |
| 624 Miladia | Mwanzo wa Ramadhani imefaradhishwa funga |
| 13 | Kushuka kwa Qur'ani |

**Mradi wa:** Muongozo Mfupi wa Muislamu **Usanifu:** Hassan Baharoun **Ubunifu na utendaji:** Taasisi ya Modern Guide **Rejea:** Kitabu cha Lataaif Maarif **cha Ibnirajab** Ahkaam Qur'an **cha Qurtubiy** Tafsiir Qur'an Adhiim **cha Ibnikathiir**

MODERN GUIDE